

## ***SURA YA OI***

Jua linachmoza kwa bali purukushani katika mtaa ambao ulikaliwa na watu masikini wenye hali duni kimaisha zilianza "Fabiano?" anaiita mama yake Fabiano.

Lakini Fabiano alikuwa ameamka anatoka kitandani kisha anaanza kukug'uta kaptura yake aliyokuwa anaivaa malanyingi hasa anapokuwa mtaani. "Namm" aliitika huku akikohowa Fabiano alikuwa mpole "leo huwendi kuchunga kondoo?" anamuuliza mama yake.

Kushoto mwanyumba yao kulikuwa na zizi lililokuwa na kondoo wengi "naenda mama" alimjibu kwa sauti Fransisca dada yake Fabiano yeye alikuwa amewahi kuamka na mama yake mapema walikuwa wakielekea wote shambani,

"sawa utafunga mlango" anampa maelekezo Fabiano anakuwa kimya kusikiliza huku akivaa kaptura yake mama yake anaondoka huku akiwa ameambatana na binti yake Fransisca.

"Mama umeniamsha mapema hata sijasali" alisema Fransisca akiwa anamlaumu mama yake alionyesha nikama ameshindwa kufanya kitu muhimu kwenye maisha yake ya kila siku,

Fabiano anatoka katika chumba chake cha kulala alipokuwa anatoka nje anaisikia sauti ikimjia masikioni mwake "rafiki yako leo atakusariti" hakushituka kwasababu ya sauti ile bali anashituka kwataarifa hiyo.

"rafiki gani!" anashangaa sauti ya namna hiyo ilikuwa inamjia malanyingi na mambo mengine aliweza kumshauri hata mama yake na yakafanikiwa kupitia sauti hiyo ambayo ilikuwa ikimjia hata katika kufanya jambo lolote alifanya kwa haraka.

Sauti ilipo mjia na alipo jiuliza hivyo picha inamjia akilini rafiki yake ambae walikuwa nae muda mwingi machungoni "Gamalieli" analitaja jina la **GAMALIEL** huku akiwa na mshangao mkubwa.

"Anataka kunifanyia jambo gani baya?" wakati akiwa anafikiria hivyo mala anaingiwa na uwamuzi wakuhairisha kwenda huko anaingiwa na sehemu ambayo ilikuwa nisehemu nyingine ya kuchungia ambayo ilikuwa na umbali kutoka hapo alipokuwa anakaa "nitaenda huko sijisikii kwenda kuchunga sehemu moja na Gamaliel,

Anaenda kufungulia zizi la kondoo nao wanatoka wengi kisha anafunga mlango wazizi huku akienda kufunga na mlango wa nyumba yao. Asubuhi ilikuwa hakuna mtu anayebakia nyumbani wote walienda kuhakikisha wanafanya kazi.